



## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

### ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

#### BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

#### MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 14 Februari, 2025.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

#### I. TAARIFA YA SPIKA:

#### II. MASWALI:

##### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

8. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Namba 8 ya mwaka 2022 kifungu cha 45 imeweka wazi kosa la kutumia majina yasiyofaa kuwaita watu wenye ulemavu.

- (a) Je, Wizara yako imechukua juhudzi zipi za kuielimisha jamii juu ya kosa hilo.
- (b) Tokea ilipoanza kwa Sheria hiyo, ni watu wangapi wamebainika kufanya makosa hayo na hatua gani zimechukuliwa dhidi yao.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

106. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:
- (a) Ni lini bustani ya kupumzikia wananchi iliyopo Jumbi - Wilaya ya Kati itakamilika.
  - (b) Ni kwa utaratibu upi wananchi watakuwa na fursa ya kuweza kuitumia bustani hii.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

27. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Vyombo vyta usafiri wa anga, baharini na hata nchi kavu vinaweza kuwa na mchango mkubwa wa kuvitangaza vivutio mbali mbali vyta utalii na historia ya nchi yetu.

Kwa kiasi gani Wizara yako imelipa umuhimu na mazingatio suala hili.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

40. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tunaelekeea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Nchi yetu siku chache zijazo.

- (a) Je, Wizara yako imejipanga vipi kuhakikisha inawachukulia hatua kali za kisheria Waandishi wa Habari watakaoandika habari zenyet viashiria vyta uvunjifu wa amani.
- (b) Je, Wizara yako ina uhakika upi kwamba sheria zilizopo zinakidhi haja na matakwa ya kuwajibisha Waandishi wa Habari wanaoandika taarifa za uchochezi.

131. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Je, ni lini fikra na wazo la kuwa na makumbusho ya kumbukumbu ya michezo na sanaa itazaliwa Zanzibar.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

77. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na changamoto ya wanafunzi wa Mtule kufuata masomo katika skuli ya Kitogani kwa zaidi ya kilomita 5, hali inayopelekea usumbufu na kupunguza ufanisi wa masomo ya wanafunzi hao.

- (a) Ni lini taarifa hii iliwahi kuifikia Wizara yako.
- (b) Ni lini wanafunzi hao watejengewa skuli iliyo karibu na wanapoishi.
- (c) Ni ipi kauli ya Wizara yako kwa wananchi wa kitongoji cha Mtule.

99. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kiasi gani Wizara inapambana katika kutatua changamoto ya uhaba wa walimu wa mafunzo ya amali ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kimtaala.

**Wizara ya Afya:**

116. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tathmini kwa sasa iko vipi juu ya ongezeko la watu wenye tatizo la afya ya akili.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

49. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kuna tofauti gani ya uwepo wa Bahari Kuu na uwepo wa Maji ya Kitaifa kwa muktadha mzima wa uelewa wa uchumi wa buluu.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016 na Kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,  
14 Februari, 2025.

  
(Raya Issa Msellem)  
**KATIBU WA BARAZA.**